Uhakika Wa Mambo Katika Ulimwengu Huu Unategemea usahihi wa Taarifa Anazosikia Mtu Na Hivyo Humpa maarifa na Kumjengea Imani Impayo Mtu Maisha. Ufanisi Na Ubora Wa Mambo Yote Katika Maisha Unategemea Umakini Na Ustadi Wa Maandalizi Yake. Hakika Maandalizi Ndiyo Mbegu Ya Matokeo Yote Yanayotarajiwa Na Mwanadamu.

Ndoa Ni Taasisi Ya Kimbingu Iliyoanzishwa Duniani Na Mungu Kwa Ajili Ya Wanadamu Kulitimiza Kusudi Lake. Ndoa Ni Wito Ambao Kuingia Inahitajika Maandalizi Ya Kufaa Yanayojenga Ubora Na Ufanisi Kwa Viwango Vya Kimungu Kwa Kusudi Lake.

**Mashauri 8 Ya Uchumba Mtukufu** Yamebeba Nguvu, Majibu Na Suluhisho Juu Ya Mambo Yahusuyo Maandalizi Ya Ndoa Isiyo Na Mashaka, Majuto Wala Usaliti Bali Iliyojaa Furaha, Upendo Na Utoshelevu.

Uchumba Mtukufu Ni Ule Unaodhihirisha Tabia Ya Kimungu Ndani Ya Wahusika Na Kwa Wale Washuhudiao. Uchumba Unaotoa Ufunuo Katika Kutawala **Maamuzi**, Unaothibitisha **Maandalizi** ya Wanandoa Halisi, Unaoanzisha **Mchakato** Wenye Mwelekeo, Unaofuata **Kanuni** Sahihi, Ufunzao Kutathmini **Gharama,** Unaopima **Ukomavu** Kamili, Unaoepuka Sababu Za **Migogoro,** Na Unaoogopa **Makosa.**

Tuna Uhuru Wa Kuamua Mambo Katika Maisha, Lakini Tukishaamua Hatuna Uhuru Wa Kukwepa Matokeo Ya Maamuzi Yetu Kamwe

Ni Siri 8 Zenye Nguvu Na Utukufu Wa Mungu Utazifahamu Uzisomapo Na Kuzitenda. Endelea